**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 5, Issue 1, 2022**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Uhusiano wa Kifahiwa katika Leksia za Kîîtharaka: Mtazamo wa Leksika Pragmatiki

*Kimathi Mwembu[1*], Allan Mugambi[2] & Timothy Kinoti M'Ngaruthi[3]*

[1] Chuo Kikuu cha Tharaka, S. L.P. 193– 60215, Marimanti, Kenya.
[2] Chuo Kikuu cha Chuka, S.L.P. 109– 60400, Chuka, Kenya.
[3] Chuo Kikuu cha Embu, S.L.P. 6– 60100, Embu, Kenya
[*] ORCID ID: https://orcid.org/0000-0001-9687-2484; Barua pepe ya mawasiliano: kwamwembu@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.859**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*26 Septemba 2022*

**Istilahi Muhimu**:

*Kîîtharaka, Leksia, Uhusiano Wa Kifahiwa, Ubadili Maana, Leksika-Pragmantiki.*

**IKISIRI**

Makala haya yanalenga kubainisha jinsi fahiwa zinavyohusiana katika leksia za Kîîtharaka kwa kuzingatia mtazamo wa leksika pragmatiki.Ubadili maana katika leksia mbalimbali husababisha kutokea uhusiano wa kifahiwa katika leksia moja, na kati ya leksia mbili au zaidi. Katika makala haya, ubadili maana unaozua uhusiano wa kifahiwa katika leksia za Kîîtharaka umeangaziwa. Data ya kimsingi kutoka wazungumzaji asilia wa Kîîtharaka, imechanganuliwa kwa kutumia nadharia ya Leksika-Pragmantiki. Matokeo yanabainisha kwamba ubadili maana ukitokea katika leksia za Kîîtharaka, mahusiano ya kifahiwa yafuatayo hutokea: uhusiano wa kipolisemia, kihomnimia, kisinonimia, kihaiponimia, kimeronimu na kiantonimu. Makala haya yanahitimisha kwamba, maana ya leksia huwa na uhusiano na maana nyingine ya leksia iyo hiyo au leksia nyingine tofauti. Pia, kuna mwingiliano baina ya maana kimatumizi na maana kimuktadha ya leksia.

**APA CITATION**

Mwembu, K., Mugambi, A. & M'Ngaruthi, T. K. (2022). Uhusiano wa Kifahiwa katika Leksia za Kîîtharaka: Mtazamo wa Leksika Pragmatiki. *East African Journal of Swahili Studies*, *5*(1), 341-352. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.859.

**CHICAGO CITATION**

Mwembu, Kimathi, Allan Mugambi and Timothy Kinoti M'Ngaruthi. 2022. "Uhusiano wa Kifahiwa katika Leksia za Kîîtharaka: Mtazamo wa Leksika Pragmatiki". *East African Journal of Swahili Studies* 5 (1), 341-352. https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.859.

**HARVARD CITATION**

Mwembu, K., Mugambi, A. & M'Ngaruthi, T. K. (2022) "Uhusiano wa Kifahiwa katika Leksia za Kîîtharaka: Mtazamo wa Leksika Pragmatiki", *East African Journal of Swahili Studies*, 5(1), pp. 341-352. doi: 10.37284/jammk.5.1.859.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.859

**IEEE CITATION**

K. Mwembu, A. Mugambi, & T. K. M'Ngaruthi, "Uhusiano wa Kifahiwa katika Leksia za Kîîtharaka: Mtazamo wa Leksika Pragmatiki", *EAJSS*, vol. 5, no. 1, pp. 341-352, Sep. 2022.

**MLA CITATION**

Mwembu, Kimathi, Allan Mugambi & Timothy Kinoti M'Ngaruthi. "Uhusiano wa Kifahiwa katika Leksia za Kîîtharaka: Mtazamo wa Leksika Pragmatiki". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 5, no. 1, Sep. 2022, pp. 341-352, doi:10.37284/jammk.5.1.859.

## UTANGULIZI

Kwa mujibu wa uainishaji wa Guthrie (1970), Kîîtharaka kimo katika kundi la lugha za Kibantu zinazopatikana katika eneo la Kati ya Kenya. Katika mgawo huu, Kîîtharaka kimepewa kodi ya E50. Bennet (1977, 1985) anasema kwamba kundi hili la lugha za Kibantu za eneo la kati ya Kenya hujulikana kama Lugha za Thagicu. Bennet (keshatajwa) anaendelea kusema kuwa lugha za jamii-lugha ndogo ya Thagicu ni Kîîtharaka, Kikuyu, Kikamba, Kiembu na Kimeru. Kîîtharaka kina lahaja nne za kijiografia: Gîgatue, Kîîgoki, Gîntugî na Kîthagicû (Bible Translation and Literacy, 2010).

Makala haya yanadhamiria kujadili uhusiano wa kifahiwa katika maneno. Mahusiano ya kifahiwa katika maneno hutokea katika hali ya usinonimia, uhaiponimia, na uantonimia. Uhusiano wa kifahiwa ni kukaribiana kwa maana katika leksia kama ilivyo katika sinonimu, ujumuishaji wa maana katika haiponimia, na hali ya kukinzana kama inavyojitokeza katika antonimu(Kreidler, 1998). Kuna aina mbili kuu za uhusiano wa kifahiwa: uhusiano wa kifahiwa unaoeleza utambulisho na ujumuishaji wa maana za maneno; na ule unaodhihirisha ukinzani na kujitenga kwa maana za maneno. Kundi la kwanza linashirikisha maneno yenye maana zinazosawiana au zinazojumuishwa pamoja. Kundi la pili linahusisha fahiwa za maneno yenye ukinzani wa maana, au maana zinazojitoa katika maneno mengine (Cruse 2004).

Maana huwa na muundo wa kisaikolopedia unaoshirikisha maana msingi na fahiwa zake zote (Geeraerts, 2006). Fahiwa ni mfumo wa uhusiano wa kiisimu uliopo baina ya farida moja ya kileksia na farida nyingine. Licha ya mahusiano ya vikoa vya maana, leksia huweza kuwa na uhusiano kiasi kwamba maana ya leksia moja inasaidia kufahamika na labda hata kusababisha kuwepo kwa leksia nyingine katika mfumo wa lugha husika. Uhusiano mwingine ni wa kidhahania ambao hutokana na uwezo wa kiutambuzi unaohusisha dhana moja na nyingine kupitia mfananisho wa kisitiari. Leksia fulani hueleweka vizuri kupitia kuelewa mambo mawili muhimu; uhusiano wake na ulimwengu halisi, na uhusiano wake na leksia nyingine katika mfumo wa lugha husika (Nasr, 1980).

## UHUSIANO WA KIPOLISEMIA

Upolisemia ni hali ya kuongezea maana kwa maneno yaliyomo katika lugha. Idadi ndogo ya msamiati katika lugha hupanuliwa maana kwa njia inayorejelea dhana mbalimbali zenye uhusiano wa kihistoria. Uhusiano wa kipolisemia hutokea wakati leksia fulani hupanuka kimaana na kuanza kutumika kurejelea dhana mpya huku maana asilia ikiendelea kutumika (Kipacha, 2005; Mwangi na Mukhwana, 2011).

Kuna tofauti kubwa baina ya polisemia na homonimia. Hata hivyo, kuna baadhi ya wataalamu wanaotumia neno jumuishi 'visawe' wakirejelea polisemia na homonimia kwa pamoja. Wataalamu hawa huzingatia kigezo cha maumbo pekee, bila kuangalia chanzo na uhusiano wa kihistoria wa leksia husika. Homonimia huwa ni maneno yenye maumbo sawa lakini maana na chanzo chake huwa tofauti (Ogutu, 2013). Sifa mahususi za polisemia ni kwamba: huwa ni maneno yenye maana zaidi ya moja; maana hizo huwa na historia moja; na kuna umbo moja la neno. Umahususi dhahiri wa polisemia ni kuwa na uhusiano wa kihistoria. Hii ndiyo sababu Habwe na Karanja (2004), wanasema kuwa polisemia ni uhusiano ambapo kuna umbo moja la neno lenye maana mbalimbali zinazohusiana kihistoria. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya uhusiano wa kipolisemia katika Kîîtharaka.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.859

**Jedwali 1: Mifano ya leksia zenye upolisemia katika Kîîtharaka.**

| Leksia | Maana ya Kimsingi | Maana za Ziada |
|---|---|---|
| *Kîongo* ‘kichwa’ | 1. sehemu ya mwili wa mnyama au binadamu inayoshikana na shingo ambayo ina masikio, macho, midomo,taya, nywele na ubongo. | 2. kiongozi wa familia<br>3. mume<br>4. 4.kiongozi wa kundi fulani<br>5. sehemu ya mbele ya chombo cha usafiri k.v gari<br>6. sehemu ya mbele ya nyumba ya biashara<br>7. sehemu tangulizi ya habari |
| *riitho* ‘jicho’ | 1. kiungo cha mwili cha kuonea | 2. mwakilishi wa kundi fulani<br>3. taa ya gari, pikipiki, trektaau baiskeli |

Katika jedwali hili, leksia *kîongo* ina fahiwa saba zinazohusiana kihistoria. Kwamba, maana ya pili hadi saba zinatokana na maana ya kwanza. Maana ya kwanza au ya kimsingi ya leksia *kîongo* ‘kichwa’ ni kuongoza sehemu nyingine katika mwili wa binadamu au mnyama. *Kîongo* ‘kichwa’ huongoza sehemu nyingine za mwili wa binadamu au mnyama kwa kuwa sehemu hii ina kiungo muhimu ambacho ni ubongo. Kupitia mchakato wa ubadili maana, neno *kîongo* ‘kichwa’hutumiwa kurejelea kila sehemu ya kitu au asasi ambayo inachukua nafasi ya kuongoza kama inavyojitokeza katika mifano ya sentensi (1).

1(a) **Kîongo** gia Karigû i gîgûtuma

‘**Kichwa** cha Karigû kinauma’

(b) **Kîongo** kia **mûciî** ûyû nûû?

‘**Kichwa** cha **familia** hii ni kipi?’

(c) **Nkingo** îtikûrûkaga **kîongo**.

‘S**hingo** haiwezi kupiku **kichwa**’

(d) Kanini nwee athuurwa ari **kîongo** gia gîkundi gietû.

‘Kanini ndiye amechaguliwa kuwa **kichwa** cha kikundi chetu’

(e) Thimû îrîendua goro ta **kîongo** gia **nkaarî**.

‘Simu inauzwa bei ya juu kama **kichwa** cha **gari’**

(f) Kînyua aakîte puroti yake **kîongo** gîonka.

‘Kînyua amejenga ploti yake **kichwa** pekee’

(g) Kîongo kia ntheto kîriuga ata?

‘**Kichwa** cha habari kinasema nini?’

Katika (1), maana za neno *kîongo* katika (1b) hadi (1g) zimehusiana na maana ya msingi ya neno hilo katika (1a). Katika (1b), kiongozi wa familia anaitwa *kîongo* ‘kichwa’ kwa kuwa anatekeleza jukumu la kuelekeza familia katika kufanya maamuzi kama inavyofanyika wakati kichwa cha binadamu; kupitia ubongo kinavyodhibiti na kuelekeza sehemu nyingine za mwili. Katika (1c) mume anaitwa *kîongo* ‘kichwa’ naye mke anarejelewa kama *nkingo* ‘shingo’. Ufananisho huu unatokana na majukumu yanayotekelezwa na kila mmoja katika ndoa. Katika jamii ya Atharaka, mwanamume ndiye anayepaswa kuwa mstari wa mbele ili atoe mwelekeo katika mahusiano ya kindoa. Hali hii ya kuwa mbele katika kutoa mwelekeo inamfanya mume kuwa kichwa cha ndoa, huku bibi akiwa shingo.

Maana ya neno *kîongo* katika (1d) inarejelea mtu anayechukua nafasi ya kuongoza kikundi chochote cha watu. Mtu anayechukua nafasi hii huitwa *kîongo* ‘kichwa’ kwa kuwa anapaswa kuelekeza kikundi kama vile kichwa cha binadamu au mnyama kinavyoelekeza sehemu nyingine za mwili.

Katika (1e) sehemu ya mbele ya gari inaitwa *kîongo* ‘kichwa’. Sehemu hii inafananishwa na kichwa cha binadamu kwa sababu nne kuu: Kwanza, injini inayozalisha nishati ya kuendesha gari inapatikana katika sehemu hii. Vilevile, thamani ya gari inachukuliwa kuwa kwenye injini yake. Pili, usukani unaoelekeza gari upo katika sehemu hii. Tatu, aghalabu sehemu hii ndiyo inayoongoza wakati gari linapoendeshwa, isipokuwa wakati wa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.859

kurudi nyuma. Nne, taa za kumulikia ili kutoa mwangaza kwa dereva; ambazo Watharaka wanaziita *meetho* ‘macho’ zimo katika sehemu ya mbele ya gari. Kichwa cha binadamu kina ubongo unaoelekeza sehemu nyingine za mwili kama usukani wa gari ufanyavyo. Macho ya binadamu au mnyama mwingine yapo kwenye kichwa, vivyo hivyo taa ‘macho’ ya gari yapo kwenye kichwa cha gari. Thamani ya gari inahusishwa na injini kama vile heshima na umaarufu wa mtu fulani unavyohusishwa na uwezo wake wa kutumia ubongo wake.

Mahusiano ya kipolisemia katika (1f) yanatokana na hali ya kuwa sehemu ya mbele ya nyumba za kufanyia biashara katika mji hujengwa ikiwa na milango inayoangalia barabara. Si ajabu kusikia watu wakisema fulani ana nyumba yenye ‘vichwa viwili’, hususan ikiwa ploti yake imo mkabala na barabara kutoka pande mbili. Sehemu hii pia huwa na vyumba vikubwa ikilinganishwa na vile vingine vianavyokuwa sehemu ya nyuma. Hii ndiyo sehemu inayoonekana na mtu akiwa kwenye barabara, hususan ikiwa nyumba hiyo si ya ghorofa. Uhusiano wa sifa za sehemu hii ya nyumba ya kufanyia biashara na zile za kichwa cha binadamu huifanya kuitwa ‘kichwa’.

Upolisemia katika (1g) unatokana na maneno tangulizi katika mkusanyiko wa habari. Maneno tangulizi huitwa ‘kichwa’ kwa kuwa huchukua nafasi ya kwanza kabisa katika habari zilizoandikwa. Maneno haya huandikwa kwa namna ya kumvutia msomaji, msikilizaji, au mtazamaji. Maneno tangulizi humwelekeza na pia kumwongoza msomaji, msikilizaji, au hata mtazamaji wa runinga; ili ajue ni habari za aina gani anatarajia kupata. Kama vile kichwa cha binadamu kilivyo muhimu katika utambulisho wa sura ya kila mmoja, ndivyo kichwa cha habari kinavyotambulisha ujumbe uliopo. Kwa ufupi, fahiwa saba katika neno *kîongo* ‘kichwa’ zinahusiana kihistoria. Zote zimetokana na sehemu ya mwili wa binadamu au mnyama ambayo inaitwa kichwa. Mfano mwingine wa uhusiano wa kipolisemia unaosababishwa na ubadili maana katika leksia za Kîîtharaka upo katika matumizi ya neno *riitho* ‘jicho’ katika (2).

2(a) **Riitho** ria Gîtuura ria ûmotho rirî na mwimba

‘**Jicho** la Gîtûûra la kushoto lina uvimbe’

(b) Gwegû i gwû **riitho** rietû ndeni ya mbunge îno.

‘Wewe ndiwe **jicho** letu katika bunge hili’.

(c) Nkaarî ya baba îrîmûrîka na **riitho** rîmwe.

‘Gari la baba linamulika kwa kutumia **jicho** moja’.

Katika (2) maana za neno *riitho* ‘jicho’ zinahusiana. Katika (2a) shughuli kubwa ya jicho la mwanadamu au mnyama ni kuona. Katika hali hii, neno *riitho* ‘jicho’ limetumiwa kwa maana ya mwakilishi wa watu. Kazi ya jicho ni kuona kwa niaba ya viungo vingine vya mwili. Kwa hivyo, katika (2b) mwakilishi anafanya kazi ya kuona upungufu wa serikali; na pia kuona kwamba raslimali zimetengewa watu wake kama inavyopaswa. Katika (2 c) maana ya neno *riitho* inahusiana na ile ya (2 a) kwa kuwa kazi ya taa ya gari ni kumulika ili dereva aone barabara vizuri wakati wa usiku. Katika hali hii, jicho la binadamu linafanya kazi karibu sawa na ile ya taa ya gari. Hii ni kwa sababu, mtu huongozwa na mwangaza unaopitia kwenye macho yake hadi ubongoni ambapo tafsili mwafaka hufanyika.

Katika uhusiano wa kipolisemia, mzungumzaji na msikilizaji hutumia maarifa ya ufahamu na kanuni za kipragmatiki ili kutambua ni fahiwa gani ya neno inahitajika kutumiwa katika muktadha fulani. Yaani, wakati mtu anapotumia maneno yenye upolisemia, inambidi kujenga dhana ya dharura kuhusiana na leksia husika. Mzungumzaji au msikilizaji akijenga dhana ya dharura, anasimbua maana inayotokana na dhana ya dharura hiyo katika leksia husika.

## UHUSIANO WA KIHOMONIMIA

Homonimu ni uhusiano ambapo leksia hufanana katika muundo wa kifonetiki lakini zina maana tofauti.Maneno katika uhusiano wa kihomonimu huwa yanafanana katika maumbo lakini yakiwa na maana tofauti. Kufanana kiumbo huwa ni tukio la kisadfa. Homonimu huwa hazina maana zenye uhusiano wa kihistoria wala chanzo kimoja (Gichuru, 2020; Ogutu,2013). Homonimu ni leksia mbili au zaidi katika lugha moja zenye kuandikwa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.859

sawa lakini zenye maana tofauti. Homonimu huwa na sifa ya kutamkwa sawa, na vilevile, kuandikwa kwa njia sawa. Umbo la homonimu huwa na homofoni na pia homografu. Homofoni ni maneno yanayotamkwa sawa lakini yenye maana tofauti zisizohusiana. Nayo homografu huwa ni maneno yanayoendelezwa kwa namna moja lakini maana zikiwa tofauti kabisa, na pia hakuna uhusiano wa kihistoria unaopatikana katika maneno ya aina hii. Homofoni na homografu huwa ni kitu kimoja katika Kĩĩtharaka, Kiswahili na lugha nyingine za kibantu ambazo othografia na matamshi ya maneno yanalingana. Ifuatayo ni mifano ya homonimu (homofoni na homografu) katika Kĩĩtharaka.

3. (a) 1. *kîraka* /keraka/'aina ya mawele' – aina ya nafaka zinazosagwa unga wa kupika uji au ugali.

2. *kîraka*/keraka/ 'kiraka'- kipande cha kitambaa kinachoshonewa mahalipalipochanika.

(b) 1. *îria /eria/* 'maziwa'–kiowevu kizito na cheupe kutoka kwenye titi la mnyama au binadamu.

2. *îria /eria/* 'bahari/ziwa'- eneo kubwa la maji.

3.*îria /eria/* 'kwekwe' – mimea inayomea mahali isipotakikana na inasumbuamimea halali.

(c) 1. *mûcinka /mociŋka/* 'mjinga'-mtu asiye na maarifa.

2. *mûcinka/mociŋka/* 'bunduki'- silaha ya kufyatulia risasi.

Katika (3), kila jozi ya maneno, maendelezo na matamshi ni sawa isipokuwa maana. Katika (3a) neno *kîraka* lina maana mbili tofauti kabisa. Hakuna uhusiano uliopo baina ya nafaka aina ya mawele na kitambaa cha kurengeta mahali palipochanika. Maana ya kwanza ya neno *kîraka* inatokana na jina la mzungu Clerk ambaye alikuwa mtafiti wa kilimo katika eneo la Tharaka katika miaka ya sitini na sabini. Ni yeye aliyeanzisha upanzi wa aina hii ya muwele unaozaa mawele aina ya *kîraka*. Maelezo zaidi kuhusu asili ya aina ya mawele kwa jina *kîraka* yamo katika sehemu ya etimolojia jumuishi.Vivyo hivyo, hakuna uhusiano wa kihistoria wa maana tatu katika maneno *îria* (3b). Kila neno lina maana yenye chanzo tofauti kabisa na nyingine. Maziwa, bahari na kwekwe havihusiani hata kidogo. Ni sadfa tu kwamba maendelezo ya maneno haya yanafanana. Maneno *mûcinka* (3c) yamekopwa kutoka Kiswahili na kuingizwa katika Kĩĩtharaka yakiwa na maana ile ile. Maana ya silaha na mtu asiye na maarifa. Katika Kiswahili, neno 'mjinga' ndilo liliasilishwa ili liwe *mûcinka*, huku neno 'mzinga' likipewa matamshi *mûcinka* baada ya kuasilishwa kifonolojia. Homonimu hutokea wakati maneno mawili yenye matamshi na maendelezo tofauti yanapoanza kutamkwa na kuendelezwa kwa njia sawa; huku yakiendelea kurejelea dhana tofauti (Rahmati, 2015). Mabadiliko ya aina hii huenda yakachukua muda kutokea. Matumizi mwafaka ya maneno katika uhusiano wa kihomonimu hufanikishwa na kipengele cha dhana ya dharura katika kukarabati maana ya leksia (Omoke na wenzake, 2018). Matumizi ya maana sahihi ya kila seti ya homonimu katika (6a,b,c), huhusisha ujenzi wa dhana ya dharura ya maneno: *kîraka, îria na mûcinka*.

## UHUSIANO WA KISINONIMIA

Maneno mawili au zaidi ambayo maana zake zinakaribiana sana huwa katika uhusiano wa kisinonimia. Maneno haya pia hujulikana kama visawe (TUKI, 1990). Usinonimia ni uhusiano wa kileksia ambapo leksia mbalimbali za lugha moja huwa na maana sawa (Gichuru, 2020). Kwa mujibu wa Crystal (2010), sinonimu ni visawe vya dhana moja. Visawe hivi huwa na uhusiano A= [ B1, B2, B3…Bn] kiasi kwamba A ina maana sawa na aina zote za B. Kwa mfano, neno *ûguru* 'ujinga' lina maana sawa na *ûritu*, *ûnoko, ûtaku* na *gwaa*. Usinonimia ni uhusiano ambapo leksia moja au zaidi huwa na uwezo wa kutumika kama mbadala wa nyingine katika muktadha maalum . Sinonimia zinaweza kubadilishana nafasi kwa kutegemea muktadha wa mazungumzo au maandishi ( Rahmati 2015). Uhusiano wa kisinonimia husababishwa na ukopaji wa msamiati, tofauti za kilahaja, tofauti za maeneo ya kijiografia, taaluma, jinsia, dini na mpito wa wakati ( Habwe na Karanja, 2004). Ifuatayo ni mifano zaidi ya sinonimu katika Kĩĩtharaka:

4. (a) ***ûgûta/ûthao*** 'uzembe'

**Ûgûta/ûthao** bwake butimûreka athoma bwega

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.859

'**Uzembe** wake utamzuia kusoma vizuri'

(b) ***ûnene/waramu*** 'upana'

Nyaga akarora mwatû wake agîtûmagîra mbarî îra îrî na **ûnene/waramu**

'Nyaga atarina mzinga wake akianza upande ulio na **upana**'

(c) ***gûmîîru/ûcamba*** 'ujasiri'

**Gûmîiru/ûcamba** bwake bukamûtethia kûrûa na maitha

'**Ujasiri** wake utamsaidia kupigana na adui'

(d) ***wana/ûnyi*** 'ujana'

Antu ba ûkûrû bûnini baagîrue gûceria ûtonga îgita ria **wana/ûnyi** bwao

'Watu wanapaswa kutafuta mali wakati wa **ujana** wao'

Mifano ya maneno yaliyokolezwa rangi na kisha kuandikwa kwa italiki katika (4a, 4b, 4c) yana uhusiano wa kisinonimia. Kwa mujibu wa Richards na Schmidt (2002), leksia zilizo katika uhusiano wa kisinonimia huwa na fahiwa sawa, au kuwa karibu sawa. Kutokana na uhusiano wa namna hii, *ûgûta* na *ûthao* ni maneno mawili ambayo yanabadilishana nafasi bila kuathiri maana ya sentensi katika (4a). Vilevile, fahiwa za maneno *ûnene* na *waramu* haziathiri maana iliyokusudiwa katika (4b). Hali ni iyo hiyo katika (4c). Maneno *gûmîiru* na *ûcamba* yametumika kwa njia ya kisinonimia. Kadhalika, maneno *wana* na *ûnyi* yametumika kwa njia ya mpishano huru. Muktadha wa matumizi ya sentensi (9d) unaruhusu maneno *wana* na *ûnyi* kurejelea faihiwa sawa. Hata hivyo, katika muktadha tofauti na huu, maneno *wana* na *ûnyi* si sinonimia. Akishadidia kauli hii, Winiharti (2010), anasema kwamba kuna baadhi ya maneno ambayo huwa na uhusiano wa kisinonimia katika muktadha mmoja lakini hali isiwe hivyo katika muktadha mwingine. Hali kama hii inajitokeza katika mfano ufuatao:

5. (a) Ntikwenda ***wana*** bwaku. 'Sitaki **upuuzi** wako.'

(b) * Ntikwenda ***ûnyi*** bwaku. 'Sitaki **ujana** wako.'

Jozi ya maneno *wana* na *ûnyi* katika (5) haiwezi kuwa katika uhusiano wa kisinonimia kwa kuwa neno *ûnyi* haliwezi kubadilishana nafasi na neno *wana*. Muktadha wa matumizi ya neno *wana* katika (5a) unazua fahiwa tofauti na ile ya *ûnyi*. Maana inayojitokeza inarejelea hali ya ujinga, kiasi kwamba ni sahihi kukataa *wana* 'upuuzi' au 'ujinga' wa msemewa, lakini si sahihi kusema kwamba unakataa *ûnyi* 'ujana' wake kama ilivyo katika (5b). Wazungumzaji wa lugha fulani huwa na uwezo wa kufahamu kile msemaji anamaanisha wala si kile amekitamka. Yaani, ubadili maana katika leksia hujitokeza kutokana na umaanisho wa kimazungumzo. Leksia mbili zenye uhusiano wa kisinonimia haziwezi kubadilishana nafasi kwa njia ya moja kwa moja katika miktadha yote bila kubadilika kwa fasili ya usemi (Saeed, 2016; Stringer, 2019). Kwa hivyo, uhusiano wa kisinonimia katika seti ya maneno mawili huwezi kukosa dosari. Usinonimia hutegemea muktadha wa matumizi.


## UHUSIANO WA KIHAIPONIMIA

Hurford (2007), ametoa kijelezo cha haiponimia kwa kusema kwamba ni uhusiano baina ya maneno mawili, ambapo maana ya mojawapo ya maneno hayo hujumuisha maana ya neno jingine. Kwa mfano, maana ya neno ***maketha*** 'mavumo' huwa katika uhusiano wa kihaiponimia na maneno *ndengû* 'adesi', *ncûgû*'mbaazi', *mwere* 'mawele', na *nthoroko* 'choroko'. Vilevile, maneno *njoka* 'nyoka', *cimba* 'simba', *mbiti* 'fisi', na *mpuria* 'kifaru' yamo katika uhusiano wa kihaiponimia na neno ***nyamû*** 'mnyama'. Katika mwelekeo sawa na huu, neno ***îtunda*** 'tunda' lina uhusiano wa kihaiponimu na maneno *yembe* 'embe',*îbabaî* 'papai', *îbeera*' 'pera', na *îcunkwa* 'chungwa'. Uhusiano wa kihaiponimia ni zao la mchakato wa ubanaji maana katika leksia. Uhusiano wa kihaiponimia katika Kîîtharaka unajitokeza katika (6) na (7).


This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.859

6.




7.




Kupitia ubadili maana, haiparonimu *maketha*'mavuno' (6) na*nyamû*'mnyama'(7) zimepanuka maana ili kujumuisha maana za maneno yaliyo chini yake katika uhusiano wa kihaiponimu. Uhusiano wa kihaiponimu huwa na neno-jumuishi ambalo hujulikana kama haiparonimu. Chini ya haiparonimu kuna haiponimu (Habwe na Karanja, 2004; Gichuru, 2020). Haiponimu ni maneno ya daraja ya chini ambayo maana zake hujumuishwa katika maana ya haiparonimu. Maneno katika daraja ya chini huwa katika uhusiano wa kihaiponimu-nyenza; na ndiyo sababu yanarejelewa kama haiponimu-nyenza ( Cruse, 2004; Winiharti,2010). Kwa mfano, katika (6) neno *maketha* ni haiparonimu inayojumuisha *ndengu*, *ncûgû*, *mwere*, na *nthoroko*. Nayo leksia *mwere* ni haiparonimu ya *kîraka*, *ciakaûngi* na *mûtûntû*. Katika (7), haiparonimu *nyamû* imejumuisha *njok*a, *cimba*, *mbiti* na *mpuria* kama maneno ya daraja ya chini kwenye uhusiano wa kihaiponimu. Haiponimu za leksia *njoka* 'nyoka' ni: *gîîko* 'swila', *mpuua* 'bafe' na *kîrea-manyore* 'mamba'.

Kutokana na mifano katika (6) na (7) kuna mambo matatu yanayojitokeza kuhusiana na uhusiano wa kihaiponimu. Kwanza, haiponimu za haiparonimu moja huwa na uhusiano unaofanya kila moja iwe mwenza wa nyingine katika ushirika. Hii ndiyo maana haiponimu za haiparonimu moja huitwa haiponimu-nyenza ( Winiharti, 2010). Kwa mfano, katika (6) *ndengu*, *ncûgû*, *mwere*, na *nthoroko* ni haiponimu-nyenza chini ya haiparonimu *maketha*. Jambo jingine linalojitokeza ni kuwa, katika haiponimia, maneno huwa na uhusiano wima, kiasi kwamba yanawekwa katika miundo ya kidaraja ndani ya mfumo wa akili kuhusu leksikoni (Stringer, 2019). Kwa mfano, katika (7) kuna neno

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.


East African Journal of Swahili Studies, Volume 5, Issue 1, 2022
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.859

la daraja ya juu ambalo ni *nyamû*, daraja la kati ambapo kuna *njoka* ‘nyoka’, na daraja la chini kabisa linalojumuisha aina zote za *njoka* ‘nyoka’. Mwisho, haiponimu za vitu hai kama vile mimea na wanyama huwa na sifa ya uelekezi shuruti. Sifa hii inajitokeza hivi: kwamba ikiwa kuna uhusiano baina ya vitajwa katika daraja ya kwanza na ya pili, na baina ya daraja la pili na la tatu, basi uhusiano huo upo baina ya daraja la kwanza na la tatu. Kwa mfano, ikiwa nyoka (*njoka*) wote ni wanyama (*nyamû*), na bafe (*mpuua*) wote ni wanyama (*nyamû*), kwa hivyo, bafe (*mpuua*) wote ni wanyama (*nyamû*).

## UHUSIANO WA KIMERONIMU

Uhusiano baina ya maana fulani ambayo ni sehemu ya maana nyingine hurejelewa kama uhusiano wa kimeronimu. Yaani ni uhusiano wa ‘sehemu ya’ katika kitu kamili ( Stringer, 2019). Kwa mfano, *njara* ‘mkono’ na *kûgûrû* ‘mguu’ ni meronimu za *mwîrî* ‘mwili’, sawa na vile ilivyo kwamba *mîri* ‘mizizi’ na *mpong’i* ‘matawi’ zilivyo meronimu za *mûtî* ‘mti’. Uhusiano wa kimeronimu huwa ni wa kihadhi. Meronimu na sinedoche hukaribiana sana. Hata hivyo, kuna tofauti kiasi kwamba sinedoche huwa ni mbinu ya kiisimu ambayo hutumiwa kwa wingi kama lugha ya kitamathali ya kila siku. Kwa upande mwingine, meronimu ni uhusiano wa kileksia katika sinedoche (Ogutu, 2013; Stringer, keshatajwa). Uhusiano wa kimeronimu umejitokeza katika leksia za Kĩĩtharaka kama ifuatavyo:

8.




Leksia *MBÛRI* ‘MBUZI’ kama ilivyo katika (8) imo katika uhusiano wa kimeronimu na leksia *mbûri*, *ng’ondu* na *ng’ombe*. Hii ni kwa sababu maana ya maneno haya ni sehemu ya maana ya MBÛRI. Katika Kĩĩtharaka, mzungumzaji akitaja neno MBÛRI huwa anarejelea vitu vitatu:Kwanza, anarejelea *mbûri* ‘mbuzi’,ambaye ni mnyama wa kufugwa nyumbani anayefanana na swala. Pili, anarejelea pia, *ng’ondu* ‘kondoo’ aliye mnyama mwenye mkia ulio na mafuta mengi na mwili wenye manyoya mazito; hufugwa nyumbani. Tatu, anamaanisha *ng’ombe* ‘ng’ombe’ ambaye ni mnyama wa nyumbani anayefanana na nyati; hutumiwa kutoa maziwa na kufanya shughuli kama vile kukokota jembe (TUKI, 2004). Katika mwelekeo huu, maana ya leksia *mbûri*, *ng’ondu* na *ng’ombe* inajipata ikiwa sehemu ya maana ya MBÛRI. Hii ni kwa sababu kupitia ubadili maana, neno MBÛRI limepanuka kimaana kwa kujumuisha maana ya *mbûri* ‘mbuzi’, *ng’ondu* ‘kondoo’ na *ng’ombe* ‘ng’ombe’.

## UHUSIANO WA KIANTONIMU

Kwa mujibu wa (TUKI, 1990), antonimu ni neno ambalo maana yake ina uelekeo tofauti na neno jingine. Kwa hivyo, uhusiano wa kiantonimu unahusu uelekeo tofauti wa maana za maneno. Richards na Schmidt (2002), Cruse (2004) na Stringer (2019) wanasema kuwa: antonimu ni jozi ya maneno yanayochukuliwa kuzua maana kinzani. Kuna aina nne kuu za antonimu (Hurford na wenzake,2007; Kreidler, 1998). Kĩĩtharaka kimedhihirisha aina hizi kwa njia ifuatavyo:

### Antonimu za Viwango

Aina hizi za antonimu huelezea ukinzani kwa kutumia uhusiano wa kimizani. Ukweli wake huamuliwa na mzungumzaji kwa misingi ya uhusiano wa kimizani. Antonimu za viwango ni za aina tatu. Kwanza, kuna antonimu za mkingamo ambazo hudhihirisha kiwango kikubwa cha udhahania, huku zikiwa na sifa ya ufafanuzi

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.859

mwingi. Kwa mfano, maneno *ûraja- ûkubî* 'urefu-ufupi' na *ûûthû -ûrito* 'wepesi-uzito' ni antonimu za mkingamo. Antonimu hizi zinajitokeza katika Kiîtharaka kwa njia zifuatazo:

8 (a) *Mûtî um**uraja** ûtibua akubî na nyûmba-Mûtî ûm**ûkubî** ûtibua akubî na nyumba*.

'Mti mr**efu** hautafaa karibu na nyumba- mti m**fupi** hautafaa karibu na nyumba'.

(b) Mûrigo wake n'ûm**ûûthû**-Mûrigo wake n'ûm**ûrito**

'Mzigo wake ni ***mwepesi***-Mzigo wake ni ***mzito'.***

Ukinzani wa maneno katika (9) ni wa kidhahania kwa sababu ni mzunguzaji pekee anayeweza kuwa na ukweli wa, *ûraja* 'urefu'' au *ûkubî* 'ufupi' wa mti unaorejelewa. Vilevile, mizani anayotumia kuamua *ûraja* au *ûkubi*, ama *ûûthû* au *ûrito* wa mzigo ipo katika nafasi yake ya kuamua. Pia, msikilizaji hubidi kupata ufafanuzi wa ukingamo katika antonimu hizi.

Antonimu za udhanifu wa kihisia ni aina ya pili ya antonimu za viwango. Aina hizi za antonimu huwa zinahusishwa na hisia. Kwa mfano; *gana-mûrio* 'chungu-tamu' na *mûrugutîra-mpeo* 'joto-baridi' ni antonimu za udhanifu wa kihisia. Mzungumzaji hutumia hisia zake kukadiria kinyume katika seti za maneno ya aina hii. Zingatia mfano katika (10).

10. (a) Mûkwajî ûyû ûrî na **gana** mono-Mûkwajî ûyû ûri na **mûrio** mono.

'Muhogo huu ni **chungu** sana-Muhogo huu ni **tamu** sana'.

(b) Kûrî na **mûrugutîra** îmunthî-Kûrî na **mpeo** îmunthî.

'Kuna **joto** leo-Kuna **baridi** leo'.

Uhusiano wa maneno katika antonimu za udhanifu wa kihisia ni ule wa mwendelezo wa kutoka kiwango kimoja hadi kingine. Kwa mfano, katika (10) kuna mwendelezo wa muhogo kuwa chungu hadi kufika kiwango cha utamu kwa kutegemea hisia za yule anayeonja. Kufikia mwisho wa kuhisi hali moja, ni mwanzo wa kuhisi kinyume chake.

Aina ya mwisho ya antonimu za viwango hujulikana kama antonimuza mwingiliano-pishani. Antonimu za aina hii hutoa nafasi ya kutathmini. Aidha, zinatoa maelekezo kuhusu hali fulani. Kwa mfano, *wega-ûthûku* 'uzuri -uovu'; *kîao-ûnyamû* 'huruma-ukatili' ni antonimu za mwingiliano-pishani. Uhusiano wa kiantonimu wa maneno haya unajitokeza katika Kĩĩtharaka kama ifuatavyo:

11. (a) Kîrimi akarîwa **wega** bwake ntugû ikaaya-Kîrîmi akarîwa **ûthûku** bwake ntugû ikaaya.

'Kîrîmi atalipwa **uzuri** wake siku za baadaye-Kîrîmi atalipwa **uovu** wake siku za baadaye'.

(b) Kîao gîake gîtikorokîthira-ûnyamû bwake bûtikorobûthira.

**Huruma** zake hazitawahi isha-**Ukatili** wake hautawahi isha

Uhusiano wa kiantonimu katika (11a) unapatia msikilizaji nafasi ya kutoa tathmini ili afikie uamuzi kwamba msemewa (Kîrîmi) alitenda uzuri au kinyume chake. Ikiwa basi alitenda uzuri atalipwa baadaye, na ikiwa alitenda kinyume chake pia atalipwa, lakini kwa njia isiyo ya kupendeza kama wakati ametenda uzuri. Kinyume cha huruma ni ukatili. Katika (11b),wazungumzaji wana nafasi ya kutathmini tabia ya mtu fulani ili waamue kama ni mwenye huruma au kinyume chake. Kwa njia hii, antonimu hizi zinamwelekeza msikilizaji kufahamu hali fulani. Hii ni kutokana na hatua ya kutathmini maneno yaliyo katika uhusiano wa kiantonimu wa aina hii.

## Antonimu za Kiutoano Kamilifu

Hizi ni antonimu ambazo kutokea kwa hali moja, kunamaanisha kwamba moja kwa moja kinyume cha hali hiyo hakijatokea. Matumizi ya neno la upande mmoja yanajumulisha kukosekana maana ya neno lenye kinyume chake (Cruse, 2004 Stringer, 2019). Kutokea kwa hali moja, bila shaka ni kukosekana kwa kinyume chake. Maneno *mwoyo-gîkuû* 'uhai-kifo' na *inga-rugûra* 'funga-fungua'' huwa na ukinzani wenye maana jumulishi. Yaani, kinyume cha maana ya maneno haya ni jambo lenye ulazima wa kutotea. Tazama mfano katika (12).

12(a) *Nkarî arî **mwoyo***. 'Nkarî yu **hai**'

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.859

(b) Nkari n'ûmû**kuû.** 'Nkari ni **mfu**'

Maana katika (12a) inajumulisha maana katika (12b) kwa njia ya ukinzano. Kutokea kwa hali katika (a) ni kukosekana kwa hali katika (b). Kinyume cha kuwa hai ni kuwa mfu. Ikiwa 'Nkarî yu hai', bila shaka 'hajakufa'. Uhusiano wa antonimu za kiutoano kamilifu zinadhihirisha kwamba hakuna vile hali zote mbili zinaweza kutokea kwa pamoja, wala hali ya ubaki kutokea. Hii ni kwa sababu, uhusiano wa aina hii unatenga kabisa pande mbili za nyanja moja (Teufel, 2014). Hali kama hii ndiyo inatokea katika (13), ambapo maneno *inga-rugûra* 'funga-fungua' yanatumiwa kwa njia kinzani ili kuonyesha kwamba kuna pande mbili za nyanja moja zilizotenganishwa kabisa licha ya kuwa na uhusiano wa dhana mbili husika. Zingatia mfano huu;

13(a) ***Inga*** *mûrango*. '**Funga** mlango'

(b) ***Rugûra*** *mûrango.* '**Fungua** mlango'

Kufunga mlango ni kinyume cha kufungua. Hali hizi mbili zimo katika nyanja moja katika akili ya mzungumzaji ambayo inahusu mlango, lakini katika uhusiano kinzani.

**Antomu za Uelekeo**

Maneno yaliyo katika uhusiano huu yanadhihirisha ukinzani unaohusisha upande. Kinyume katika leksia kama hizi huwa katika uhusiano wa pande mbili kinzani ambazo zimo katika uelekeo ulionyooka (Cruse, 2004; Winiharti, 2010). Maneno *ûrio-ûmotho* 'kushoto-kulia', *ncû-îthi* 'njoo-enda' *naiti-naîgûrû* 'kusini-kaskazini' ni mifano ya antonimu za uelekeo. Mifano ya matumizi ya antonimu za uelekeo ipo katika sentensi (14) na (15).

14. Karîmi ambîîria kûrîmîîra njara ya **ûrio**, Kaini nwee aambîîrie njara ya **ûmotho**.

'Karîmi anzia kulima kutoka upande wa kulia, naye Kaini aanzie kushoto'

15. ***Ncû*** *aaga, kana arî,* ***îthi*** *naara!* '**Njoo** hapa, ama hapana, **enda** huko!'

Sentensi hizi zinadhihirisha kinyume cha uelekeo ulionyooka. Katika (14) Karîmi akianza kulima kutokea upande wa kulia, Kaini anapaswa kuanzia upande kinzani katika uhusiano wa kunyooka. Vivyo hivyo, katika (15), 'njoo' na 'enda' ni maneno yanayotumiwa kuashiria pande kinzani kimwendo.

**Antonimu za Uhusiano-Jozi**

Kinyume katika antonimu za uhusiano-jozi huhusu jozi ya maneno ambayo ni lazima yote yawepo wakati sawia ili kila neno liwe na thamani ya ukweli. Kwa mfano, jozi za maneno *mûka/mûrûme* 'mke/mume' na *kooba/koobithania* 'kopa/kopeshana' ni antonimu za uhusiano-jozi. Mfano wa matumizi ya antonimu za uhusiano-jozi upo katika (15) na (16).

15. *Ndagûrîrwe nguo i* ***muka*** *wakwa*. 'Nilinunuliwa nguo na **mke** wangu'

16. *Njeeri*, agû***kooba*** *mbeca kuuma kîrî Kamau*. 'Njeeri, ame**kopa** pesa kutoka kwa Kamau'

Kinyume cha mke ni mume. Kwa hivyo, katika (15), mwanamke fulani hawezi kusemekana kuwa mke bila mwanamume fulani kuwa mume wake. Hii ndiyo sababu hali ya kinyume inajitokeza katika (15). Maana inayojitokeza ni kuwa, aliyenunuliwa nguo si mwingine bali ni mume. Ukweli wa mwanamke aliyenunua nguo kuwa mke wa mtu fulani upo sawia na kuwepo mtu anayesemekana ni mumewe. Katika mwelekeo sawa na huu, kauli ya (16) inadhihirisha kinyume cha uhusiano-jozi. Mtu hukopeshana wakati kuna kinyume chake. Yaani, pawe na mtu wa kukopa. Mifano mingine ya antonimu za uhusiano-jozi ni kama vile:

17(a) *mwandîkwa- mwandîkani* 'mwajiriwa-mwajiri'

(b) *mûgûrwa-mûgûrani* 'bibi arusi-bwana arusi'

Shughuli ya kuajiri hufanywa na *mwandîkani* 'mwajiri'. *Mwandîkwa* 'mwajiriwa' hufanya kazi aliyopewa na mwajiri. Katika (17a), kutokea kwa mwajiri kunasababisha moja kwa moja kuwepo kwa kinyume chake. Haiwezakani mtu fulani kuajiriwa bila kuwa na mwajiri wake. Mfano katika (17b), unadhihirisha uhusiano wa kiantonimu baina ya *mûgûrwa* 'bibi arusi' na *mûgûrani* 'bwana arusi'. Kinyume cha 'bibi arusi' ni 'bwana arusi'. Uhusiano wa leksia hizi mbili ni wa kiantonimu za

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.859

uhusiano-jozi. Kutajwa kwa dhana inayorejelewa na neno moja kati ya haya mawili, kunaashiria moja kwa moja kuwepo kwa dhana inayorejelewa na neno lililo kinyume chake. Mwanamwali hurejelewa kwa jina bibi arusi wakati kuna mwanamume aliyeridhia kumuoa, na kinyume chake.

## HITIMISHO

Makala haya yanahitimisha kwamba, kupitia michakato ya ubadili maana, leksia za Kĩĩtharaka huwa na fahiwa zinazohusiana. Uhusiano huu huwa ni wa kujumuisha maana kama ilivyo katika hali ya upolisemia, usinonemia, uhaiponimia na uhomonimia, au kujitenga kimaana kama ilivyo katika hali ya uantonimu. Mtazamo wa kileksika pragamatiki ni mwafaka katika uchunguzi wa aina hii, kwa kuwa umetumika kuelekeza katika kubaini maana ya kimsingi ya leksia na vilevile maana ya kimuktadha. Aina hizi mbili za maana huwa na mchango mkubwa katika ujenzi wa uhusiano wa kifahiwa katika leksia za Kĩĩtharaka.

## MAREJELEO


Bennett, R.P. (1977). Dahl'sLaw andtheThagicu. In*African LanguageStudies*, Vol. VII, pp. 127-159.

Bennett, R.P. (1985). DhaagicwLifeStages: A StudyinParadigmaticReconstruction. I *HistoryinAfrica*, Vol 12 pp. 11-28.

Bible Translation & Literacy (2010). *KĩĩrĩkanĩroKĩĩyerû*. Nairobi: Bible Translation andLiteracy (E.A)

Cruse, D.A. (2004). MeaninginLanguage: AnIntroductiontoSemanticsandPragmatics. 2nd edn. Oxford: oxford University Press.

Crystal, D. (2010). *The Cambridge Encyclopediaofthe English Language*, 3rd ed. Cambridge: Cambridge University Press.

Geeraerts, D. (2006). *CognitiveLinguistics: BasicReadings*. Berlin: JeanetteLittle&John Taylor.

Gichuru, T. M. (2020). Mabadiliko ya Maana za Leksia za Kiswahili: Mtazamo Linganishi wa Kale na Kisasa. Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Guthrie, M. (1970). *The Classificationof Bantu Languages*, London: International African Institute.

Habwe, J. &Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Hurford, J.R. (2007). *Semantics: A Coursebook*. *2nd edn*. Cambridge: Cambridge University Press.

Mwangi, P.,&Mukhwana, A. (2011). *Isimujamii*. Nairobi: Focus Publishers Ltd.

Kipacha, A. (2005). Utangulizi wa Lugha na Isimu. OSW 101. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. https://www.researchgate.net/publication ilidondolewa tarehe 20/2/2022.

Kreidler, E. W. (1998).*IntroducingSemantics.* London: Routledge.

Nasr, R. (1980). *The EssentialofLinguisticsScience*. Essex: Longman Group Ltd.

Ogutu, G. (2013). Athari za Sheng katika Dini ya Kikristo: Mtaa wa Umoja. Tasinifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Omoke, J.N., Barasa, D.,&Basweti, N. (2018).Ekegusii Sense Relationsin a Lexical Pragmatic Theoritical approach. *International Journal of Academics and Research*, Vol 1:1 Pp 15-21

Rahmati, F. (2015). SemanticShift, Homonyms, Synonyms and Auto-antonyms. *WalliaJournal*Vol 31 (53), pp.81-85.

Richards, J.C.,& Schmidt, R. (2002). Longman Dictionary of LanguageTeaching and Applied Linguistics. 3rd Edition. London: Pearson Education Limited.

Saeed, J. L. (2016). *TheoriesofLexicalSemantics*. Oxford: Oxford University Press.

Stringer, D. (2019). *LexicalSemantics: Relativity and Transfer*. Indiana: IGI Global Ltd.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.859

Teufel, S. (2014). *Lexical Semantics: Antonymy and Sentiment Detection*. Cambridge: Cambridge University Press.

TUKI.(1990). Kamusi *Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: Educational Publishers and Distributers Ltd.

TUKI.(2004). Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Dar es Salaam: Educational Publishers and Distributers Ltd.

Winiharti, M. (2010). Sense Relations in Language Learning in *Humaniora* Vol.1 No.1 pp 100-106.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.